# FORM FOUR TERM ONE EXAM 2017

## WONGOZO WA KUSAHIHISHA 102/2

**Majibu ya ufahamu**

**SCHOOLS NET KENYA**
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

# WONGOZO WA KUSAHIHISHA 102/2

**Majibu ya ufahamu**

a) Ipe makala haya kichwa mwafaka (alama 1)
Wajibu wa kaunti/kazi ya kaunti lx 1=1

b) Je? Kaunti inawajibikaje katika kuhudumia wananchi (alama 3)
i) Kutoa huduma za afya kwa umma kama kujenga hospitali na vifaa vinavyotakikana
ii) Kusimamia masuala ya uchukuzi pamoja na kukarabati barabara,
iii) kuimarisha nyenzo za uzalishaji mali kama kilimo, uvuvi, ufugaji na ukuzaji wa Mimea. 3x 1=3

b) Utawala wa kaunti unaweza kupunguza vipi maafa yanayotokea kutokana na mapuuza ya mwanadamu(alama 3)
i. kubuni sheria za barabarani pamoja na kukarabati
ii. kutoa huduma muhimu za afya
iii. kuimarisha usalama
iv. kuthibiti matumizi ya dawa za kulevya 3x1

c) Bunge la kitaifa lina wajibu gani katika serikali ya kaunti? (alama 2)
kuunda sheria za kuzipa kaunti uwezo wa kuendeleza shughuli zake

d) Ni changamoto zipi zinazoweza kukabili suala la ugatuzi nchini (alama 3)
i. Ufisadi
ii. Uhaba wa fedha za kuendesha miradi ya maendeleo
iii. majukumu ya kaunti kuingiliwa na serikali kuu
iv. Ukosefu wa wataalamu waliohitimu katika nyanja mbalimbali
3x1=3

d) Ni kwa njiani gani serikali ya kaunti inaweza kufufua uchumi wa nehi na kuinua kiwango cha maisha iii kufikia ruwaza ya 2030 (alama 2)
i. kubuni nafasi za kazi
ii. kufufua na kuanzisha viwanda vya uzalishaji bidhaa
iii. kuimarisha miundo msingi

f) (i) Uchukuzi - Kubeba mizigo na kusafirisha abiria
(ii) Ugatuzi - Ugavi wa mamlaka na rasilmali 2x 1=2

2. **UFUPISHO.**

(a) i) Simu tamba inayotumiwa katika mawasiliano ni mfano wa teknolojia mpya.
ii)Wakongwe mashambani wanaitumia kuwasiliana na wajukuu wa ugenini.
iii)Majokofu,tanuri la male viko katika vyumba vingi.
iv)Majokofu nayo huhifadhi vitu mbalimbali.
v)Trekta itumiwayo na mtu nimoja kulima ni mfano wa teknologia mashambani, kazi ya ukulima
vi)umerahisishwa na vifaa vya mashambani.
vii)Teknologia vile vile hutumiwa kukuza mimea na wanyama.
viii)Mwisho, teknologia imewezesha watu kuvumbua vitu vingi kwa hivyo, mababu zetu mashambani hutazama televisheni. (8X1)= 8

(b) i)Uundaji wa silaha kali unaoangamiza watu, mabomu ya kitinoradi yaliyowaua watu Hiroshima na Nagasaki na ambayo bado yanadhuru watu nchini Japani ni ya madhara ya teknologia.
ii) Magaidi nao hutumia teknologia kuangamiza watu.
iii) Wahalifu nao husikiza mawasiliano ya watu hata polisi.
iv) Matatizo ya kiafya yanayotokana na vyakula.
v) Ingawa mwendo wakasi ya gari la moshi linalotumia stima huweza kusababisha ajali mbaya sana.
(5x15)Utiririko alama (2)

**SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA**

(a) / e / - irabu ya mbele
- Midomo hutandazwa
- Irabu ya kati

/u / - Irabu ya nyuma
- Irabu ya juu
- Midomo huviringwa ***(Tofauti zozote mbili = alama 2)***

(b) (i) - li — kauli ya kutendea — alama 1
-a—kiishio— alama 1
(ii) Sehemu ya neno inayobeba maana kuu alama 1

(c) Alituchochea alama 1

(d) Kuonyesha swali kuonyesha ombi
Kuonyesha amri
Kuonyesha taarifa
Kuonyesha mshangao, hasira n.k. ***zozote 2 alama 2***

(e) mfano: Lili hili litatupwa alama 2

(f) Wimbo wa mama ulitufurahisha. alama 2

(g) Angali — kitenzi kishirikishi kikamilifu alama 1

Alikuwa — kitenzi kishirikishi kipungufu /ihalisi

(h) wa — kivumishi cha a unganifu alama 1

mwenye kivumishi cha pekee alama 1

(i) Karibu na — kihusishi cha mahali alama 1

hadi — kihusishi cha kiwango alama 1

(j) chagizo — zaidi

(k) Mgomba uo huo huo huo ***(mwalimu ahakiki sentensi)***

(1) (i) Hakiki sentensi (Udogo wa sabuni) nomini alama 1

(ii) Hakiki sentensi (Kisabuni kama kielezi) alama 1

(m) (i) Tunzo/zawadi/uongofu lx1 =1

(ii) Damu lx 1= 1

(n) Chumvi ichafuka<u>yo</u> si ile uizungumzia<u>yo</u> 2x1= 2

(o) Mwanasiasa shupavu amekamatwa-kishazi huru.

Aliyechochea wananchi- kishazi tegemezi. (1 x2)

(P) Uzi ungekatika ungepotea 1 x2= 2

(q) Ngeli ya i—I 1 x1=1

(r) Mofimu tegemezi- kitanda, n.k

Mofimu huru . – k.m darasa, mimi n.k

**Jinsi ya kusahihisha matumizi ya Lugha**

- Ondoa nusu ( ½ ) kwa kila kosa la sarufi (s) litokeapo kwa mara ya kwanza kwa kila kijisehemu lakini isipite nusu ya alama alizopata katika kijisehemu hicho.
- Ondoa nusu alama ( ½ ) kwa kila kosa la tahajia (h) litokeapo mara ya kwanza hadi makosa sita katika swali lote yaani:

**ISIMU JAMII**

(a) (i) Diglosia — hali ya kuwa na lugha mbili tofauti katika taifa, zilizo na majukumu tofauti k.m Nchini Kenya Kiswahili ni lugha ya taifa, Kiingereza ni lugha ya ofisini/rasmi

(ii) Misimu — Ni maneno yanayoibuka katikajamii na kukaa kwa muda mfupi; yakikaa sana usanifishwa na kuwa lugha sanifu.

(b) (i) Kukopa maneno kutoka lugha nyingine.

(ii) Msamiati wa kitekinolojia kufumbuliwa.

(iii) Misimu husanifishwa na kuwa Kiswahili sanifu.

(iv) Kushikanisha maneno kuunda nomino ambata.

(v) Utohozi — Uswahilishaji wa maneno.

(vi) Matumizi ya akronimu Runinga,Ukimwi n.k ( al. 1x 3 =3)

(c) (i) kuna kuchanganya ndimi.

(ii) Kuna kuhamisha ndimi.

(iii) Kiswahili sanifu hakitumiki.

(iv) Kuna utohozi wa maneno.

(v) Matumizi mengi ya misimu.

(vi) Lugha ya kumkosea mtu heshima hujitokeza.

(iii)Hujaa mizaha

(iv)Kuna matumizi ya lakabu. ( al. 1x 5 =5)

**Jinsi ya kusahihisha Isimu Jamii**

- Ondoa nusu ( ½ )alama kwa kila kosa la sarufi (s)litokeapo kwa mara ya kwanza kwa kila kijisehemu lakini isipite nusu ya alama alizopata (si alizotengewa) katika kijisehemu hicho.
- Ondoa nusu ( ½ ) alama kwa kila kosa la hijai (h) litokeapo kwa mara ya kwanza hadi makosa matatu yaani (3 x ½ = 1 ½ )